
**TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
(TaSUBa)**

WITO KWA WASANII NA VIKUNDI KUSHIRIKI KATIKA

**TAMASHA LA 36 LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
KUANZIA TAREHE 23 HADI 30 SEPTEMBER 2017**

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo inapenda kuwakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kwa ujumla kuomba kushiriki kwa kufanya maonyesho katika tamasha la 36 la kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambalo litafanyika katika viwanja vya taasisi (**TaSUBa – Bagamoyo**) kuanzia tarehe **23 hadi 30 Septemba 2017**.

Tamasha hili limekuwa na malengo mbalimbali kama vile kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wasanii na vikundi vya Tanzania na mataifa mengine kupitia warsha na maonyesho mbalimbali.

Tamasha hili hujumuisha aina mbalimbali za sanaa kama vile **Ngoma, Maigizo, Muziki, Sarakasi, Mazingaombwe, Vichekesho** n.k pamoja na maonyesho ya sanaa za ufundi (**Exhibitions**).

TaSUBa inawakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi ili kuweza kushiriki katika tamasha hili kongwe la sanaa na utamaduni wa Mtanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia;

Barua pepe: bagamoyofest@gmail.com, info@tasuba.ac.tz au tasuba@habari.go.tz

Tovuti: www.tasuba.ac.tz

Namba za Simu: +255(0) 754 310 425, +255(0) 655 840 405, +255(0) 713 297626, au +255(0) 787 537 771